

SHIRIKA LA KIMATAIFA UNICEF WAKISIRIKIANA NA RITA WAKIFANYA UFUATILIAJI WA USAJILI WA VYETI

Ufuatiliaji huo umefanywa na Bw. Alex Kabunga kutoka UNICEF wakiambatana na Mwinyijuma Moshi kutoka RITA wakiambatana na mwenyeji wao Alphonse Chilimo katika ukaguzi wa obo ya 3 na ukaguzi wa obo ya 4 utanza aprili.

Aidha katika ufuatiliaji huo wametembelea baadhi ya maeneo ya Kata za Paranga, Kidoka, Chemba pamoja na Gwandi.

Katika ufuatiliaji huo wamebaini changamoto zifuatazo:

1. TAARIFA ZA MTOTO kuunganishwa na taarifa za Mzazi kama vile
Jina la Kwanza: (hapa hujazwa jina la motto tu)
Jina la Pili : (Hapa hujazwa kama mototo ana majina mawili)
Makosa yaliyofanyika ni kwenye Jina la Pili ambapo mjaza taarifa badala ya kujaza jina la pili la motto yeye amejaza jina la baba ambapo haitakiwi.
2. Kutokujaza taarifa kikamilifu kwa mfano: Aina ya kizazi kama ni mmoja, mapacha au zaidi ya wawili pamoja na hali ya kizazi kama ni Mfu au Hai
3. Kutokujaza postikodi ya makazi ya Mtoto, Baba au Mama.
4. Kutokuwekwa saina za watoa taarifa za watoto
5. Kujazwa taarifa za wazazi jina la kwanza na la kati tu.
6. Kurudiarudia kuandika herufi moja iliyokosewa badala ya kufuta na collection fluid.
7. Kuacha wazi eneo la umri.
8. Wajazaji wengine hawakupatiwa mafunzo.
9. Wenye vitabu vya miongozo ya ujazaji wa fomu kuhama na vitabu hivyo badala ya kuyiacha kituo husika.
10. Kutokusajili vyeti kwa muda mrefu tofauti na wastani wa vizazi kwa mwezi.

USHAURI KWA WATOA HUDUMA:

1. Taarifa za Mtoto zisiunganishwe na za mzazi.
2. Taarifa zote zijazwe kikamilifu kwani kumbukumbu hizi ni za muhimu ambapo baada ya mda zitakusanywa na kusaniwa ili zikatunzwe kwenye ghala kumbukumbu la takwimu Taifa.
3. Kama mzazi ana majina mawili tu basi ijazwe jina la kwanza na la mwisho.
4. Kama umekosea kujaza fomu usirudie rudie bali ufute na collection fluid tu na ukikosea kujaza cheti basi usikitoe ujaze kingine kwakuwa cheti hakiruhusiwi kufutwa.
5. Umri wa wazazi usiachwe wazi na kama umeshindwa kuukadiria basi andika 99.
6. Wajazaji ambao hawakupatiwa mafunzo wawaulize wenzao jinsi ya kujaza na endapo nafasi ya kuwafundisha itatokea watapatiwa mafunzo hayo.

7. Wenye vitabu vya viongozo wanapo hama kituo wasiondoke na vitabu hivyo.
8. Kama wana nchi wapo mbali na maeneo ya kutolea huduma inashauriwa watumishi wa afya wanapoenda outreach wabebe na vitabu vya usajili wav yeti.

USHAURI KWA UONGOZI.

1. Ufuatiliaji uendelee kwa mapana zaidi.
2. Miongozo itolewe copy ili kuwapatia wasio na miongozo
3. Stationary zitolewe kama collection fluid na pen.
4. Vitabu vipya visambazwe kulingana na mahitaji.

Aidha tunachukua nafasi hii kuwapongeza watoa huduma wote kwa ushirikiano.

Imeandaliwa na Alphonse Chilimo